# HALMASHAURI YA WILAYA YA MPWAPWA

## TAARIFA YA MAFANIKIO YALIYOPATIKANA KUTOKA KWA WALENGWA WA TASAF KUPITIA SIMULIZI ZAO.

**UTANGULIZI.**

Mpango wa Tasaf wa kunusuru kaya maskini wilayani Mpwapwa umeweza kuwazungukia baadhi ya wanufaika wa mapango huo kujua mafanikio yaliyopatikana kupitia mpango wa Ruzuku kwa walegwa. Zifuatazi ni baadhi ya simulizi za walengwa katika kata nne (Mpwapwa mjini-ilolo,Lupeta-lupeta,Luhundwa-ikuyuna Malolo-malolo).

**1.KATA YA ILOLO**

Mtendaji wa Kijiji cha Ilolo Bi **Mwanaisha Bakari** alielezea Malengo ya fedha za TASAF (Fedha za Walengwa zisizokuwa na Masharti na Fedha za walengwa waliofanya kazi katika miradi ambayo ipo chini ya Mpango wa TASAF).

Pia alielezea namna wananchi hao walivyoweza kubadilisha maisha yao kupitia mpango huo kwa kuboresha makazi, kuinua kipato cha familia na kuwa na uhakika wa matibabu pindi wanapo umwa kwa kuwa na bima za afya za CHF ILIYOBORESHWA ambazo huwasaidia kupata matibabu kirahisi, katika mpango wa ajira za muda Mtendaji alizungumzia jinsi walengwa walivyoanzisha mpango wa uoteshaji miti na kuigawa kwa wananchi na Taasisi kwa ajili ya utunzaji wa Mazingira.

- **JINA LA MLENGWA – EDA ELIA MAZENGO**

**Simulizi – Mwanzo;** Mlengwa alikuwa akiishi katika nyumba ndogo isiyomtosha .Ambapo alisema kuwa kabla hajaingia kwenye mpango wa Tasaf alikuwa na nyumba yenye chumba na sebule hakuwa na kitanda hivyo alikuwa akilala chini na hakuwa na chanzo cha kipato katika familia yake.

**-Hali ya sasa**

Mlengwa alianza na Mradi wa kuuza mboga za majani ,fedha aliyoipata akaanza kufyatua matofali na kuuza. Baada ya hapo akanunua bati kwa ajili ya kuanza ujenzi wa nyumba ya bati yenye ukubwa wa vyumba 3 ambayo hivi sasa anaishi na familia yake.

-Pia mlengwa amefanikiwa kununua Kitanda na Godoro na ameweza kupiga sakafu katika nyumba aliyoijenga.

***NYUMBA YA AWALI WA BI EDA MAZENGO KABLA HAJAINGIA KWENYE MPANGO.***






Nyumba ya Bi Eda Mazengo baada kuiingia Katika Mpango wa Tasaf.

-Aidha Mlengwa amefanikiwa kujiunga katika Umoja wa kusaidiana ambapo wanakopeshana kiasi cha Shilingi 30,000/= kwa miezi 2 na riba ni Shilingi 3,000/= hivyo kumuwezesha kuendelea kupata kipato kwa ajili ya matumizi ya familia.

**-Changamoto**

Changamoto aliyoipata ilikuwa ni kunyeshewa na mvua wakati wa msimu wa mvua pia kuwa na nyumba ndogo hivo kushindwa kuishi vizuri na familia. Kushindwa kupata mahitaji ya msingi ya familia kwa sababu ya kutokuwa na kipato.

**JINA LA MLENGWA – AMOSI COSMAS**

**Simulizi – Mwanzo;** Mlengwa alikuwa akiishi katika nyumba ndogo na isiyomtosha kutokana na familia aliyokua nayo.



**- Hali ya sasa**

Baada ya kuanza kupokea fedha za TASAF Mlengwa alikuwa anaweka akiba kidogo kidogo. Baada ya hapo akaanza Mradi wa kufuga Nguruwe na kuanza

kuuza nguruwe na kununua bati kidogo kidogo hadi kufikisha idadi ya bati 53. Mlengwa amefanikiwa kujenga nyumba ya vyumba 4.

-Pia Mlengwa anaendelea na mradi wa ufugaji wa nguruwe na kwa sasa ana jumla ya nguruwe 11 ambapo wakubwa ni 3 na wadogo ni 8.



Nyumba ya sasa ya Bwana Amos Kosmas baada ya Kuingia Kwenye Mapango wa Tasaf.

**-Changamoto**

Changamoto aliyoipata ilikuwa ni kunyeshewa na mvua wakati wa msimu wa mvua pia nyumba ndogo ya tembe hivo alishindwa kuishi vizuri na familia.

Kuishi na watoto watano kwenye vyumba viwili ambpo baadhi ya watoto iliwalazimu kukimbia nyumba na kwenda kupanga wakati muda wa kujitegemea ulikuwa bado hivyo baada ya kujenga nyumba mahusiano ya kifamilia yamerudi ambapo mala ya kwanza ilikuwa inawalazimu watoto wa kike na wakiume kuishi kwenye chumba kimoja.

“Ukweli mimi isingekuwa Tasaf sijui maisha yangekuwaje mwanzo nilikuwa Napata pesa kidogo na kuweka akiba ambapo pesa ziliongezeka na kuwa nyingi haapo ilinilazumu kununua bati na kupaua nyumba yangu ya vyumba vitatu na

sebule hivyo nakili bila Tasaf  maisha yangekuwa mabaya sana" aliongea .Pia bwana Cosmas enaendelea kufuga nguruwe

Idadi ya nguruwe 11 wa bwana Amos Kosmasi





**JINA LA MLENGWA: PHILEMON MSAFIRI MASIMEGA**

**Simulizi – Mwanzo;** Mlengwa ni mtu asiyeona pia hakuwa na kipato cha kuweza kumudu mahitaji ya familia kutoka na ulemavu wake wa kutokuona.

**- Hali ya sasa**

Mlengwa baada ya kuingia katika program ya TASAF na kuanza kupokea fedha alianza kwa akibaya fedha hiyo kidogokidogo na baadae akununua mbuzi jike 10 na kuazima bebeeru wawili kwa jirani yake wanaozalisha mapacha. Kwa muda wa miaka 2 aliweza kuzalisha mbuzi 150. Akauza mbuzi 80 na kupata fedha kiasi cha Tshs 4,500,000/= akaenda mnada wa Mlembule na kununua Ng'ombe 10, majike 8 na dume 2 kwa Tshs 3,000,000/= Hadi sasa Ng'ombe hao wamezaliana na kufikia 19 anaowafuga mbali na makazi yake. Pia mlengwa ameweza kujenga nyumba ndogo mahali anapofuga mbuzi pamoja na kujenga uzio baada ya kuuza mbuzi wengine. Hivyo mlengwa amebakiwa na mbuzi 28, wakubwa 25 na wadogo 3 anaoendelea kuwafuga. Kupitia mradi huu mlengwa anaendelea kunufaika kwa kupata kipato kinachomuwezesha kumudu mahitaji ya familia.

***Banda la mbuzi la malemgwa Philimon Masimega Kijiji cha Ilolo Mtaa wa Majumbasita***





## 2. KIJIJI CHA LUPETA

Bi Rucy Chilatu ni mkazi wa kijiji cha Lupeta na ni mnufaika wa Mpango wa Tassaf,aliyeanza kupata Fedha hizo za ruzuku ya mashari Tsh 20,000 kwa mwenzi na pesa za wanafunzi wawili Ths 8000 kwa mwezi .Aliitumia pesa ya Tasaf kwa kulima shamba la alizeti la ekari tatu na baada ya kuvuna alizeti hizo alipata gunia kumi na mbili(12) na kuziuza ,pesa aliyoipata alinunua Bati 27 kwa kusaidiana na Familia yake alifyatua tofali na kujenga nyumba ya vinne .Pia mlengwa anaendelea na ufugaji wa Nguruwe wanne.





**3. KIJIJI CHA IKUYU**

**JINA LA MLENGWA: CHUKIA MTUNA**

**Simulizi – Mwanzo;** Mlengwa alianza kufuga mbuzi 6 baada ya hapo akuuza mbuzi na kununua bati 16 alizotumia kuezekea nyumba mpya yenye ukubwa wa vyumba 3.aliyoijenga kwa kutumia vyanzo vingine vya mapo vya kifamilia, Pia fedha ya TASAF imemsaidia kuendeleza kilimo ambacho mazao aliyouza alitumia kufyatua tofali kwa ajili ya umaliziaji wa ujenzi wa nyumba.Hata hiyo Mlengwa anaendelea na ufugaji na kwa sasa ana mbuzi wawili na pesa hiyo imemsaidia kukata Bima ya Afya kwa ajili yake na Familia yake.



**JINA LA MLENGWA: EVELINA ATHUMAN NGOMOLE, KITINGIJI CHA MTAKUJA**

**Simulizi – Mwanzo;** Mlengwa alikuwa anaishi kwenye nyumba ya tembe, hivi sasa amejenga nyumba ya bati na anaishi na watoto 5. Changamoto aliyoipata ilikuwa ni kunyeshewa na mvua kutokana na nyumba aliyokuwa akiiishi mwanzo(tembe). Hivi sasa mlengwa anaendelea na mradi wa ufugaji wa kuku. Pia kupitia fedha za TASAF amelima shamba la ukubwa wa ekari tatu na kununua mbegu ya karanga kwa ajiri ya kupanda.



**JINA LA MLENGWA: WITNESS OMARY NGOMOLE KITONGOJI CHA MTAKUJA**

**Simulizi – Mwanzo;** Mlengwa alinunua mbuzi 11, mbuzi wa nne wakafa, waliobaki akauza na kununua bati 10 alizoekekea nyumba yake ya vyumba vitatu, kwa kupitia fedha za Tassaf aliweza kununua kuku 10 waliozaliana na kufikia kuku 28,pia amebakiwa na mbuzi watatu anaoendelea kuwafuga,hata hivyo aliweza kukodi mashamba na kulima alipopata mazao aliuza na kufyatua tofali za kujengea nyumba yake mpya na ameweza kukata Bima ya Afya CHF.





## 4.KIJIJI CHA MALOLO

- **JINA LA MLENGWA: HURUMA PETER MBUTA**

  **Simulizi –** Mwanzo;Hapo awali mlengwa alikuwa akiishi katika nyumba ya tembe baada ya kuanza kupokea fedha za Tassa Mlengwa alianza kwa kununua na kufuga nguruwe 3 na kuuza 1 akapata fedha Tshs 200,000/= ,akaanza kuweka akiba kidogo kidogo ya pesa alizokuwa akipokea TASAF. Baadaye akaweza kufyatua tofali na kujenga nyumba mpya yenye ukubwa wa vyumba 2 na kununua viti 3. Pia mlengwa ameendelea na ufugaji wa kuku wanne na nguruwe wawili.

  ***Nyumba ya awali ya Bi Huruma Mbuta.***



***Nyumba ya mpya ya Bi Huruma Mbuta.***



***Nguruwe wa Bi Huruma Mbuta wa kijiji cha Malolo***



**JINA LA MLEGWA: EVELINA NYAMBASA**

**Simulizi – Mwanzo;** Mlengwa kwa kupitia fedha ya Tassaf aliyokua akipata kwa mwezi tsh 20,000 ameweza kununua mahitaji ya mwanafunzi anayesoma sekondariNA baada ya kufaulu na kujiunga na kidato cha tano huko Songea bado anamhudumia kupitia fedha hizo Pia ameweza kufyatua tofali kununua bati 12 na kumejengea Mama yake mzazi nyumba yenye ukubwa-wa vyumba 3, na akanunua mbuzi 3 anaoendelea kuwafuga na kukata Bima ya Afya.

***Nyumba ya Bi Evelina Nyambasa aliyomjengea Mama yake Mzazi***



***Hawa ni miongoni mwa mbuzi wa tatu wa Bi Evelina Nyambasa***



# Mwisho

Imeandaliwa na: Alutha Kimbe,

Afisa TEHAMA

Mpwapwa

Imeletwa kwenu na: Shaibu J. Masasi,

Kaimu Afisa TEHAMA (W)

Mpwapwa